



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI
(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Email ded@babatidc.go.tz

Website: www.babatidc.go.tz

S.L.P 400
BABATI.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.DED/BBT/F.30/1/VOL.II/188

01.03.2023.

**WANANCHI WOTE,
BABATI**

TANGAZO

**KUFUNGULIWA KWA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA ZIWA MANYARA, BURUNGE NA
BWAWA LA BASODAA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI KUANZIA
TAREHE 01/03/2023**

Mnaarifiwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Babati imefungua shughuli za uvuvi katika ziwa Manyara, Burunge na Bwawa la Basodaa kuanzia tarehe 01/03/2023

Mnatangaziwa kuwa licha ya kufunguliwa kwa shughuli za uvuvi, Serikali itaendelea kuthibiti na kupambana na wote watakaofanya biashara na shughuli za uvuvi bila kulipa ushuru, kuwa na vibali /leseni pamoja na kutumia zana zisizokubalika katika uvuvi kama makokoro na ngalawa ambazo hazijasajiliwa, na uvuvi wa kutumia sumu.

Wafanyabiashara wote hakikisheni mnalipa ushuru wa samaki, ada na leseni za uvuvi, leseni za ngalawa, leseni za biashara ya samaki na usafirishaji wa samaki kwa viwango vya Halmashauri

Pamoja na shughuli zote, tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa CORONA zizingatiwe.

VIWANGO VYA ADA NA LESENI

LESENI YA UVUVI TSHS 20,000/

LESENI YA NGALAWA TSHS. 20,000/=

ADA YA LESENI YA KUSAFIRISHA SAMAKI NJE YA HALMASHAURI YA WILAYA TSHS. 24,000/=

ADA YA LESENI YA KUFANYA BIASHARA YA SAMAKI NDANI YA WILAYA TSHS. 10,000/=

ADA YA KUKAANGA NA KUUZA SAMAKI TSHS. 7,500/=

Kwa yeyote atakayekiuka masharti haya hatua kali zitachukuliwa dhidi yake kutokana na sheria ya uvuvi

Anna P. Mbogo

MKURUGENZI MTENDJI (W)